IB DIPLOMA PROGRAMME
PROGRAMME DU DIPLÔME DU BI
PROGRAMA DEL DIPLOMA DEL BI

M05/2/ANSWA/SP1/SWA/TZ0/XX/T

22052841

**SWAHILI *AB INITIO* – STANDARD LEVEL – PAPER 1**
**SWAHILI *AB INITIO* – NIVEAU MOYEN – ÉPREUVE 1**
**SWAHILI *AB INITIO* – NIVEL MEDIO – PRUEBA 1**

Monday 16 May 2005 (morning)
Lundi 16 mai 2005 (matin)
Lunes 16 de mayo de 2005 (mañana)

1 h 30 m

---

TEXT BOOKLET – INSTRUCTIONS TO CANDIDATES

- Do not open this booklet until instructed to do so.
- This booklet contains all of the texts required for Paper 1.
- Answer the questions in the Question and Answer Booklet provided.

LIVRET DE TEXTES – INSTRUCTIONS DESTINÉES AUX CANDIDATS

- N’ouvrez pas ce livret avant d’y être autorisé(e).
- Ce livret contient tous les textes nécessaires à l’épreuve 1.
- Répondez à toutes les questions dans le livret de questions et réponses fourni.

CUADERNO DE TEXTOS – INSTRUCCIONES PARA LOS ALUMNOS

- No abra este cuaderno hasta que se lo autoricen.
- Este cuaderno contiene todos los textos para la Prueba 1.
- Conteste todas las preguntas en el cuaderno de preguntas y respuestas.

**KIFUNGU A**

# BURUDIKA

## GAZETI LA VIJANA WA LEO

## AGIZA LEO UPUNGUZIWE 60% YA BEI

Utapenda kila toleo la gazeti hili jipya la masuala ya vijana la BURUDIKA. BURUDIKA ni gazeti litakalokupa habari motomoto za maisha ya vijana kuhusu: Muziki na Habari za Wanamuziki; Afya; Mitindo ya Mavazi; Nafasi za masomo ndani na nje ya Afrika; Michezo; Hadithi; Mashairi; Sehemu za Burudani na za Likizo; Nyota Zenu, n.k. Pia gazeti hili lina mashindano mbalimbali ya insha, mashairi na hadithi fupifupi. Wanaoshinda hupata zawadi nono.

Kuwa kijana wa kileo kwa kuagiza na kusoma gazeti la BURUDIKA linalotoka mara moja kila mwezi.

- Agiza kwa Shilingi 1,500 tu badala ya bei ya kawaida ya Shilingi 4,500.
- Pata punguzo la 60% kwa kuagiza matoleo yote 12 ya mwaka mzima.
- Utaletewa gazeti hadi nyumbani au ofisini au shuleni kwako.
- Tunakuhakikishia utafurahia gazeti letu au tutakurudishia pesa zako zote.

*USITUME PESA SASA!!!! UTALIPA BAADA YA KUPATA TOLEO MOJA.*

Jaza tu fomu hii ya maombi uitume kwa:
Mhariri mkuu, **BURUDIKA – Gazeti la Vijana wa Leo**, S.L.P. 35040, Dar es Salaam, Tanzania

✂ - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - - -

### BURUDIKA – Gazeti la Vijana wa Leo

- NDIO! Tafadhali anza kunitumia **BURUDIKA - Gazeti la Vijana wa Leo** kwa Shilingi 1,500 tu badala ya bei ya kawaida ya Shilingi 4,500 na punguzo la 60% kwa matoleo yote 12 ya mwaka mzima wa 2006.
- Najua mnanihakikishia kufurahia gazeti hili au mtanirudishia pesa zangu zote.

Jina: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Anuani: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

. . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

S.L.P: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Simu: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Barua-pepe: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

Sahihi: . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . .

**KIFUNGU B**

# KITABU CHA KUMBUKUMBU CHA JAMILA


| JULAI 2005 | | |
|---|---|---|
| IJUMAA | 1 | Safari Arusha – Nairobi, *Hoteli ya Stanley* |
| JUMAMOSI | 2 | Kupumzika asubuhi, kutembea mchana, jioni disko |
| JUMAPILI | 3 | Kupumzika hotelini na kusoma hadithi siku nzima |
| JUMATATU | 4 | Kumtembelea rafiki yangu, Wanjiru Kago |
| JUMANNE | 5 | Matembezi Nairobi, hasa Bustani ya Nyoka |
| JUMATANO | 6 | Kutembea mjini hadi mchana, jioni kwenda *Carnivore Hotel* |
| ALHAMISI | 7 | Kutembelea Kituo cha Televisheni cha KBC – Nairobi |
| IJUMAA | 8 | Mkutano wa Vijana *Kenyatta Conference Centre* |
| JUMAMOSI | 9 | Mkutano unaendelea; jioni disko *Florida 2000* |
| JUMAPILI | 10 | Safari ya kurudi Arusha |
| JUMATATU | 11 | Safari Arusha-Moshi; na kujiandaa kupanda Kilimanjaro |
| JUMANNE | 12 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| JUMATANO | 13 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| ALHAMISI | 14 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| IJUMAA | 15 | Kupanda Mlima Kilimanjaro |
| JUMAMOSI | 16 | Kushuka na kupumzika *Hoteli ya Marangu* |
| JUMAPILI | 17 | Kurudi nyumbani Arusha |
| JUMATATU | 18 | Kusherehekea miaka ishirini ya kuzaliwa kwangu |
| JUMANNE | 19 | Mapumziko na matembezi mjini Arusha |
| JUMATANO | 20 | Kwenda Serengeti na rafiki zangu |
| ALHAMISI | 21 | Serengeti kuona wanyama, ndege na mimea mbalimbali |
| IJUMAA | 22 | Serengeti |
| JUMAMOSI | 23 | Kurudi Arusha. Jioni kwenda disko *Hoteli ya Saba Saba* |
| JUMAPILI | 24 | Kupumzika nyumbani |
| JUMATATU | 25 | Kujiandaa kupanda Mlima Meru, Arusha |
| JUMANNE | 26 | Kupanda Mlima Meru |
| JUMATANO | 27 | Kupanda Mlima Meru |
| ALHAMISI | 28 | Kushuka kutoka Mlima Meru |
| IJUMAA | 29 | Mapumziko nyumbani |
| JUMAMOSI | 30 | Mapumziko nyumbani na rafiki zangu; jioni disko |
| JUMAPILI | 31 | Kujiandaa kwa safari ya Marekani |

**KIFUNGU C**

# KIBOKO NA CHURA

❶ Hapo kale, Kiboko na Chura walikuwa marafiki wakubwa. Waliishi pamoja. Wakatafuta chakula pamoja. Wakala pamoja.

❷ Siku hizo Kiboko alikuwa anaogopa sana kuyasogelea maji. Aliamini kwamba siku yoyote ambayo angeingia ndani ya mto angezama moja kwa moja. Chura yeye alikuwa hodari wa kuogelea tangu zamani. Kwa hiyo ikawa kazi yake kwenda mtoni kuteka maji ya kunywa, ya kupikia na kuoga.



❸ Kiboko na Chura walielewana sana. Siku nyingine walikuwa wakiishi kwa taabu sana. Mara mojamoja walishinda na njaa na hata kulala nayo kwa sababu hawakujua jinsi ya kuwinda. Kutokana na shida hii waliamua kwenda kutafuta kazi kwa binadamu.

❹ Kiboko akasema, "Twende tukajaribu kupata kazi kwa Bwana Zomba. Nasikia Paka ameajiriwa na huyo bwana." Walikwenda kwa Bwana Zomba na wote wakaajiriwa. Kiboko aliajiriwa kazi ya upishi, na Chura akaajiriwa kazi ya kufagia, kudeki na kuosha vyombo. Wote walifurahi sana, wakala, wakashiba na kunenepa.

❺ Siku moja Chura akamwambia Kiboko, "Kwa nini hatuichukui ile pete ya Bwana Zomba tukaiuze?" Kiboko alikataa lakini mwishoni alikubali. Hawakujua kuwa Paka alikuwa akiwasikiliza na alikwenda kumweleza Bwana Zomba. Kwa hiyo walipokwenda kuiba wakati Bwana Zomba amejifanya kuwa amelala Kiboko alikamatwa na Bwana Zomba akapigwa rungu kichwani. Chura alijaribu kukimbia lakini Kiboko alimfuata, wote wakakimbilia na kutumbukia mtoni. Mpaka leo, Kiboko anatumbukia mtoni akimtafuta Chura.

**KIFUNGU D**

# UNGEPENDA KUWA NA MBWA?

Wazo la kuwa na mbwa ni zuri. Lakini mbwa huhitaji mahali pa kuishi na pia huhitaji kupewa muda wa kuwa na mwenye mbwa.

Yohane Rafael, mmoja wa wataalamu wa mifugo katika Kituo cha Kulea Wanyama Waliopotea (KIKUWAWA) huko Mombasa alisema kuwa kama huwezi kumpa mnyama mahitaji yote anayoyataka ni bora usiwe na mnyama huyo.

Unahitaji kufikiria kwa makini sana kabla ya kukubali kuwa na mbwa. Zaidi ya mahitaji yake ya kila siku, kama vile ya kulishwa, vilevile unahitaji kumgharamia. Kwa mfano, kama mbwa akiwa mgonjwa inakubidi kulipa zaidi ya Shilingi 50,000 ili tu ujue ana tatizo gani.

Wakati mwingine wanyama kama vile paka na mbwa huonekana kwa baadhi yetu kuwa ni kama watu, kwa hiyo mahitaji yao hayatofautiani na mahitaji yetu. Bwana Yohane Rafael anasema, "Ni kweli kabisa. Unahitaji kumpa mnyama mahitaji yake yote. Kwa mfano, lazima apate chanjo."

Zaidi ya mbwa 200,000 huachwa wakizurura ovyo kila mwaka nchini Kenya, na hasa pale ambapo familia huenda likizo na hushindwa kwenda na wanyama hao, na pia hawawezi kuwaacha peke yao majumbani. Kwa hiyo, kabla ya kuwa na mbwa, ni vizuri kila mara ufahamu utakapomuweka kabla ya kusafiri.

Bwana Yohane Rafael alimalizia maelezo yake kwa kusema, "Pamoja na kwamba mara kwa mara kituo chetu cha KIKUWAWA kimefanya kampeni na kutoa matangazo kuhusu mambo hayo hapo juu, idadi ya wanyama waliotelekezwa *(be abandoned)* inaendelea kuongezeka kila siku. Kama umefikiria kwa makini kuwa na mbwa, na unafikiri unaweza kumpa mahali pazuri pa kuishi, tuandikie kwa anuani ifuatayo ya barua pepe: kikuwawa@malindi.org".